

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA SITA

05 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 05 MEI, 2022

I. DUA

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

129. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itaangalia upya mipaka ya kiutawala katika Jimbo la Makambako.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

130. MHESHIMIWA MARIAMU MADALU NYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ya Songea.

131. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kugawa Mkoa wa Tabora na kupata Mkoa wa Manonga ili kurahisisha shughuli za Kiutawala na kiuchumi.

WIZARA YA MAJI:

132. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango wa kutoa maji Ziwa Tanganyika na kuyapelekea Mkoa wa Katavi.

133. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itasambaza maji katika Wilaya ya Nkasi kutoka Ziwa Tanganyika.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**134. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE
(LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:

Je, nini mpango wa Serikali katika kuharakisha kesi za mauaji ambazo huchukua muda mrefu kusikilizwa.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**135. MHESHIMIWA SHABAN OMARI SHEKILINDI
(LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini maeneo mengi ya Mji wa Lushoto yataapimwa.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**136. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE
NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itafikisha mawasiliano ya simu katika Kata za Kinungu, Isakamaliwa, Mtungulu, Kining'inila na Itumba.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

137. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Vituo vya Dawati la Jinsia katika kila Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

138. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia Wananchi waliotwaliwa ardhi yao kwa ujenzi wa Viwanda maeneo ya Liganga na Mchuchuma.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



**DODOMA
05 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

